**`OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU**

**SHULE YA SEKONDARI LIGOMA,**
**SLP 451,**
**TUNDURU**
**12 /12/2020**

**MKOA WA RUVUMA**
**Simu na. 0685404010 /0764878697**
**Kumb. Na. LGSS/ U.KIDT.I/VOL.1**

**KWA MZAZI/ MLEZI WA ..........................................................................................................**
**S/M.........................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI LIGOMA 2021**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii kwa mwaka wa 2021, Karibu sana. Shule ya Sekondari Ligoma ipo kata ya Ligoma ,Tarafa ya Namasakata wilaya ya Tunduru, Mkoa wa Ruvuma.Shule ipo umbali wa kilomita 24 kutoka Tunduru mjini. Shule ni ya kutwa ila ina hosteli moja ya wasichana yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 48 hivyo wanafunzi wanaotoka nje ya kata ya ligoma na watakao wahi watapatiwe kipaumbele zaidi. Shule itafunguliwa tarehe 10/ 01/2021 na masomo yataanza tarehe 13/ 01/2021.

1. 0. **MAAGIZO MUHIMU YA KUZINGATIA**

A. KWA WASICHANA

i. Sketi mbili rangi ya zambarau mshono wa rinda boksi
ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi au nusu kanzu ya rangi nyeupe kwa wanaovaa hijab
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba (gidamu) jozi 1
iv. Soksi nyeupe jozi tatu
v. Sweta rangi ya bluu
vi. Sketi moja rangi nyeusi kwa ajili ya kazi za nje ya darasa
vii. Hijabu nyeupe
viii. Tisheti rangi ya kijani jeshi yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh 13000/=

B. WAVULANA

i. Suruali mbili rangi ya zambarau (**modo haziruhusiwi**)
ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba (gidamu) jozi 1
iv. Soksi nyeusi jozi 3
v. Suruali moja rangi nyeusi kwa ajili ya kazi za nje ya darasa
vi. Sweta ya rangi ya bluu
vii. Mkanda mweusi wa ngozi
viii. Tisheti rangi ya kijani jeshi yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh 13000/=

C. SARE ZA MICHEZO KWA WANAFUNZI WOTE.

i. Bukta na tisheti ya rangi ya zambarau (jezi ya mbeya city kwa wavulana) na traki suti ya mbeya city kwa wasichana
ii. Raba jozi 1

MKUU WA SHULE
LIGOMA SEKONDARI
S.L.P 451
TUNDURU
14/12/2020

1. 1. **MICHANGO KWA AJILI YA CHAKULA CHA WANAFUNZI WA KUTWA ILIYOAFIKIWA NA WAZAZI**

    i. Mahindi debe 2 kwa muhula , debe 4 kwa mwaka.
    ii. Maharage au mbaazi kilo 12 kwa muhula, kilo 24 kwa mwaka ( **kunde hazitapokelewa)**
    iii. Fedha Tsh 10000 kwa muhula kwa ajili ya kusagia, kulipa wapishi na posho ya wasimamizi was too, ( Tsh 20000 kwa mwaka ) **Fedha hii ilipwe kupitia akaunti ya benki ya** NMB

    NAMBA **<u>70910036665</u>**

    JINA LA AKAUNTI : **<u>UMOJA WA WAZAZI SHULE YA SEKONDARI LIGOMA</u>**

    **<u>NB:</u> MZAZI AJE NA RISITI YA MALIPO YA BENKI (PAYSLIP)** na michango **ilipwe kuanzia nusu muhula au mwaka mzima.**
    iv. Chumvi kilo 1 kwa muhula ( **kilo 2** kwa mwaka)
    v. Mafuta ya kupikia **lita 1** kwa **muhula** (lita 2 kwa mwaka)

1. 2. **VIFAA VYA DARASANI**

    i. Daftari kaunta book 15, **mkebe, rula, peni, kalamu na file**
    ii. Begi la kubebea daftari

1. 3. MAHITAJI MENGINE

    i Vifaa vya usafi

    Wavulana waje na jembe 1 lenye mpini, panga 1 na ndoo 1

    Wasichana waje na reki 1 , fyekeo 1 na ndoo 1.
    ii. Vyombo vya chakula ( sahani, bakuli na kikombe)
    iii. Fedha Tsh 5000/= kwa ajili ya bima ya afya kwa wasiokua na bima tu.

2. 0. **MAHITAJI KWA WANAFUNZI WATAKAO LALA HOSTELI**

    A. CHAKULA

    i. Mahindi debe 3 kwa muhula (debe 6 kwa mwaka)
    ii. Maharage au mbaazi kilo 18 kwa muhula ( kilo 36 kwa mwaka)
    iii. Chumvi kilo 2 kwa muhula (kilo 4 kwa mwaka)
    iv. Mafuta ya kupikia lita 2 kwa muhula (lita 4 kwa mwaka)
    v. Mchele kilo 6 kwa muhula ( kilo 12 kwa mwaka).
    vi. Fedha Tsh 15000/= kwa muhula ( Tsh 30000/= kwa mwaka ) kwa ajili ya kusaga, malipo ya mpishi na posho ya usimamizi wa Stoo. Fedha hii ilipwe kupitia akaunti ya

    NMB namba **<u>70910036665</u>**

    Jina la akaunti : <u>UMOJA WA WAZAZI SHULE YA SEKONDARI LIGOMA</u>

    **<u>NB:</u> MZAZI AJE NA RISITI YA MALIPO YA BENKI (PAYSLIP) na michango ilipwe kuanzia nusu muhula au mwaka mzima**

    B. MAHITAJI MENGINE YA HOSTELI

    i. Godoro futi 2.5
    ii. Shuka 2 za rangi ya **pinki na blanketi 1**
    iii. Neti au chandarua 1
    iv. Ndoo
    v. Gauni moja rangi ya blue kwa ajili ya kushindia ( mshono wa solo)
    vi. Ndala, kitana, mswaki, sabuni , taulo,kikombe,sahani, bakuli, kijiko, mafuta ya kupaka pedi, na fedha kwa ajili ya matumizi binafsi

3. 0. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu no.27 ya mwaka 1978. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu nchini hivyo mwanafunzi anatakiwa sheria zifuatazo

    i. Heshima kwa viongozi, wazazi ,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

ii. Mahudhurio mazuri katika shughuli za darasani na nje ya darasa ni lazima
iii. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
iv. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya uwepo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uwanafunzi wako.
vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote .
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

**3. . 1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE**

i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji na ulawiti, kuoa au kuolewa na ushoga
iii. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iv. Kuchochea au kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni
v. Kutumia lugha chafu( matusi) kwa wanafunzi ,walimu, wazazi /walezi na jamii kwa ujumla
vi. Kupiga ua kupigana
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa bangi na sigara
ix. Kusababisha, kupata au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
x. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
xi. Kudharau bendera ya Taifa
xii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
xiii. Makosa ya jinai
xiv. Kugoma au kukataa adhabu kwa makusudi

**3. 2. SHERIA ZA HOSTELI**

i. Marufuku kuwa na simu au laini ya simu ya mkononi
ii. Hairuhusiwi kupika, kuingia na chakula wala kula bwenini
iii. Hairuhusiwi kumkaribisha mgeni yoyote bwenini
iv. Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa
v. Unatakiwa kuhudhuria masomo ya jioni kuanzia saa 1:30 mpaka saa 4:30 usiku
vi. Hauruhusiwi kuja na nguo za nyumbani

**NB.**Zingatia kujaza fomu ya matibabu kwa kumpima mtoto wako kwenye hospitali inayotambulika na serikali

..............................................................

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
LIGOMA SEKONDARI
S.L.P 451
TUNDURU

14/12/2020

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY

LIGOMA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX. 451
TUNDURU

DATE ...........................

TO MEDICAL OFFICER

______________________

______________________

REF: REQUST FOR MEDICAL EXAMINATION

please examine the student named ______________________ as to his fitness for studying in this school. Complete this form after check up exercise

1. Age ______________________ sex. ______________
2. Blood group ______________________
3. Stool exam nation ______________________
4. Urine analysis ______________________
5. Venereal disease test ______________________
6. T.B test ______________________
7. Eye ______________________
8. Ear ______________________
9. Chest ______________________
10. Abdomen ______________________
11. Urine for pregnant test ______________________
12. Others ______________________

Addition information ( if any) e.g physical defects or impairments of arm, leg, skin, chronic infections or family disease etc.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

Icertify that above to pursue education as stated above.

Signature ................................................ Designation ................................................

Station ................................................ date ................................................

MKUU WA SHULE
LIGOMA SEKONDARI
S.L.P 451
TUNDURU

4/12/2020